

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**



**OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO ZANZIBAR**

**MUONGOZO WA UTAYARISHAJI WA MPANGO WA MAENDELEO NA  
BAJETI KWA SERIKALI KUU NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA  
MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**Machi, 2024**

---

**KAULI YA KATIBU MKUU NA MLIPAJI MKUU WA SERIKALI,  
KUHUSU MUONGOZO WA MAANDALIZI WA MPANGO NA  
BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/2025.**

Muongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali, umeandaliwa kwa kuzingatia Kanuni ya Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2021 kifungu cha 14 (1) na (2) kinachoelekeza “Wizara inayosimamia masuala ya Fedha na Mipango kutoa Muongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti mara tu Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali utakapoidhinishwa kila mwaka wa fedha”.

Watendaji Wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa, tunatakiwa kuhakikisha tunaandaa Mipango na Bajeti kwa kuzingatia Maelekezo ya muongozo huu na ukomo wa bajeti uliotolewa kwa kufuata maelekezo ya sheria, kanuni, miongozo na tararibu za matumizi za fedha za Umma.

Viongozi wa Taasisi za Umma, tunatakiwa kuwa mfano katika kusimamia shughuli za Serikali kwa kuhakikisha tunakuwa waumini wazuri wa kutekeleza malengo na mikakati ya Serikali kwa **ustawi wa wananchi**.

Aidha, napenda kuwakumbushia kuwa kila mmoja wetu kwa nafasi yake tunawajibu wa kusimamia utekelezaji wa majukumu yetu kwa ufanisi, uthubutu na uaminifu. Aidha, taasisi yoyote, ambayo inakusudia kuanzisha Sera, kuhakikisha tunafuata utaratibu na maelekezo kupitia **Muongozo wa Uandaaji na Uandishi wa Sera za Kisekta wa mwaka 2022**, uliotolewa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Sisi kama viongozi hatuna budi kusimamia misingi ya uadilifu na mkakati wa ukusanyaji wa mapato kwa kudai risiti kwa kila huduma tunayopatiwa. Hii, itaongeza ari na utayari wa wananchi na wao kulipa kodi kwa hiari.

***Ubunifu katika majukumu yetu ndio silaha ya mafanikio ya nchi yetu.*** Matumaini yangu kwenu ni kuwa tutakuwa chachu ya kuleta mabadiliko chanya kwa kuweza kusimamia uwajibikaji na nidhamu ya kazi kwa mashirikiano na watendaji walio chini yetu. Aidha, nawakumbusha kuendelea kuitumia Taarifa ya Matokeo ya Sensa ya mwaka 2022 katika Mipango yetu. Sambamba na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuleta tafsiri sahihi ya mabadiliko ya utendaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. ***Sisi tukiwa ni sehemu ya Serikali, tunatakiwa kuhakikisha wananchi wenzetu wanafurahia manufaa ya kuwa wazanzibari, kwa kuhakikisha utendaji wetu na utoaji wa huduma zetu kwao unaakisi matarajio yao kwa Serikali yetu tukufu.***

Natanguliza Shukurani zangu za dhati na nawatakia utekelezaji mwema.

Dkt. Juma Malik Akil  
**KATIBU MKUU NA  
MLIPAJI MKUU WA SERIKALI.**

## 1 MUHUTASARI

Muongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025, umeandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016, Kifungu cha 41(2) b,c na Kifungu 86(4), na Kanuni ya Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2021 kifungu cha 14 (1) na (2) kinachoelekeza “Wizara inayosimamia Fedha na Mipango kutoa Muongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti mara tu utakapoidhinishwa Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na bajeti ya Serikali kwa kila mwaka wa fedha”.

Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Kifungu 86 (4), Mamlaka hizo zinatakiwa kutayarisha Mpango na Bajeti kwa mujibu wa Muongozo huu na kuziwasilisha katika Mamlaka husika kwa kuidhinishwa.

Madhumuni makuu ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti ni kuimarisha Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanikisha Mikakati ya Maendeleo ya Taifa yaliyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026 (ZADEP), Vipaumbele vya Sekta kupitia Mpango Mkakati pamoja na Maelekezo ya Serikali Kijumla.

Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinapaswa kuandaa Mpango na Bajeti ambao unazingatia malengo, shabaha zilizowekwa kwa ufanisi. Uandaaji wa Mpango na Bajeti unajumuisha mchakato mzima na ratiba ya bajeti **Kiambatisho Namba.1 ‘Kalenda ya Bajeti kwa mwaka 2024/2025** ambayo inapaswa kuzingatwa.

Afisa Masuuli wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali wanawajibu wa kuhakikisha uandaaji mzuri wa Mipango na Bajeti kwa shughuli ambazo zimo katika maeneo maalumu ya kimkakati wa

Serikali ambayo yameainishwa katika nyaraka mbalimbali za kitaifa ikiwemo:

- i. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025;
- ii. Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) wa Miaka mitano (2021-2026);
- iii. Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050;
- iv. Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030;
- v. Mpango Mkakati wa Sekta (Strategic Plan);
- vi. Takwimu za matokeo ya Sensa ya Watu na Makaazi ya 2022.

Ikizingatiwa kuwa Bajeti ni zana inayotekeleza Mpango wa Kitaifa na kutafsiri malengo ya sera na mpango mkakati wa Sekta, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinatakiwa kuhusisha moja kwa moja uwiano huo ili kufikia malengo yaliyopangwa. Mkazo utaendelea kuwekwa katika **kugharamia Mipango ya Maendeleo pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa kutumia rasilimali za ndani** na Washirika wa Maendeleo wataendelea kuwa na nafasi ya kusaidia jitihada za Serikali katika utekelezaji wa Mipango yetu.

## **2 MAELEKEZO MAHSUSI KWA UTAYARISHAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025**

Maelekezo mahsusi yanayopaswa kuzingatiwa na Afisa Masuuli wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa wakati wa uandaaji, uwasilishaji, pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/25.

### **2.1 Mikakati ya Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato;**

- i. Afisa Masuuli anatakiwa kuimarisha usimamizi wa vituo vya makusanyo ikiwemo viwanja vya ndege na bandari kwa lengo la kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

- ii. Afisa Masuuli anatakiwa kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina kwa wakati;
- iii. Wizara na Taasisi zote za Serikali zinatakiwa kuwasilisha kwa Waziri anaehusika na masuala ya fedha ada, ushuru na tozo zote wanazozianzisha kabla ya kuanza kutumika kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 133(b) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya Mwaka 2016 (marekebisho Finance Act ya mwaka 2020) ili kuondoa mgongano wa tozo na ada baina ya taasisi moja na taasisi nyengine;
- iv. Wizara na Taasisi zote zinatakiwa kuhakikisha kuwa zinatoza ada au tozo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizowekwa;
- v. Afisa Masuuli anatakiwa kuwasilisha ORFM kila mwezi taarifa za makusanyo kutoka kila chanzo cha mapato kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa lengo la kutathmini mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali;
- vi. Afisa Masuuli anatakiwa kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa yanaingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali;
- vii. Afisa Masuuli anatakiwa kuzingatia sheria za kodi ikiwa ni pamoja na kutoza kodi ya zuio (withholding tax) na kudai risiti za kielektroniki kwa malipo yote yanayofanywa kwa wazabuni na wakandarasi;
- viii. Afisa Masuuli anatakiwa kuwajengea uwezo viongozi na watendaji kuhusu mbinu za ukusanyaji wa mapato, uzuiaji wa mianya ya upotevu na uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato;
- ix. Afisa Masuuli anatakiwa kuendelea na matumizi ya Mifumo ya Serikali ya kielektroniki kwa ajili ya ukusanyaji wa Mapato ikiwemo Zanmalipo na Mfumo wa Bajeti na Matumizi (BAMAS); na

- x. Taasisi zote za umma zinatakiwa kuleta maelezo ya kifungu cha mapato ambacho hakijapatiwa (GFS Code) kwa ajili ya kuingizwa katika mfumo kabla ya uingizaji wa taarifa za bajeti Afisi ya Rais, Fedha na Mipango.  
**Kiambatisho Namba:2** Kasma za Bajeti

## **2.2 Maelekezo ya Uandaaji wa bajeti kwa Ununuzi wa bidhaa na Huduma**

Mpango wa Ununuzi wa Mwaka unatakiwa kuandaliwa na Taasisi za Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 46(2) cha Sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma Namba 12 ya Mwaka 2016 na Kifungu cha 42 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Namba 11 ya Mwaka 2016. Katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango huo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo;

- i. Afisa Masuuli anatakiwa kuendelea na matumizi ya Mfumo wa Ununuzi (E-Procurement) na Mfumo wa kuweka kumbukumbu za Mali za Umma (Asset Register Sytem) katika kuleta ufanisi wa kazi;
- ii. Afisa Masuuli anatakiwa kuepuka kuidhinisha manunuzi yaliyo nje ya Mpango wa Ununuzi, na inapotokea hali ya dharura anatakiwa kufuata utaratibu wa manunuzi ya dharura (Emergency Procurement) kama inavyoelekezwa;
- iii. Manunuzi yote yanayohusiana na vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT Equipments) yanatakiwa kufuata vigezo (Specifications) vilivyoandaliwa na Ofisi ya Wakala wa Serikali Mtandao;
- iv. Wakati wa kuandaa bajeti, Taasisi zinatakiwa kuainisha vifungu vya manunuzi na ambavyo sio vya ununuzi;
- v. Taasisi nunuzi zinatakiwa kutumia muundo (format) rasmi wa Mpango wa Ununuzi uliotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma;

- vi. Wizara na Taasisi zote za Serikali zinatakiwa kuwasilisha Mpango kazi na Mpango wa Ununuzi kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. **Kiambatisho Namba:3** Muundo wa uwasilishaji wa mpango kazi.
- vii. Wizara na Taasisi zote za Serikali zinatakiwa kutangaza Mpango wa Ununuzi wa Mwaka ulioandaliwa, na kusubiri kupevuka (maturity) kwa Mpango huo kabla ya kuanza ununuzi kama ilivyoelekezwa katika kifungu 42(6) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Namba 11 ya Mwaka 2016;
- viii. Manunuzi yote ni lazima yaidhinishwe na Afisa Masuuli kabla ya kuanza michakato ya Ununuzi;
- ix. Manunuzi yote yaliyofikia kiwango cha zabuni (Quotation & Tenders) ni lazima kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni katika kila hatua kama ilivyoelekezwa;
- x. Taasisi zote za Serikali zinatakiwa kutumia nyaraka rasmi za zabuni (Standard Bidding Documents) zilizoandaliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma;
- xi. Mikataba yote ya zabuni inatakiwa kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio na ushauri ili kuepuka matatizo wakati wa utekelezaji wa mikataba;
- xii. Manunuzi yote yanatakiwa kufuata njia za ununuzi zilizoainishwa katika Mpango wa Ununuzi, ikitokea kuna ulazima wa kubadilisha njia ni lazima kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni;
- xiii. Endapo yatatokea manunuzi baada ya kuwasilishwa na kuidhinishwa kwa Mpango wa Ununuzi wa Mwaka, Taasisi zinatakiwa kupitia na kuboresha (Review & Update) Mpango wa Ununuzi na kuiwasilisha Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na Mlipaji Mkuu wa Serikali.



### 2.3 Uandaaji wa Bajeti ya Matumizi Mengineyo

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Bajeti ya Matumizi Mengineyo tunatakiwa kuitayarisha na kuitekeleza kwa kutarajia matokeo zaidi badala ya kuangalia gharama **“majukumu ya msingi ya taasisi yatatekelezwa bila ya kutumia gharama isipokuwa kuwepo na haja na ulazima.**

- i. Wizara na Taasisi za Serikali kuandaa Mipango na Bajeti itakayotoa mwanga wa matarajio na dhamira ya Serikali kwa wananchi ikiwemo, **kutekeleza kwa vitendo maagizo ya Serikali yanayotolewa na Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** katika hotuba zake katika maeneo yote anayopitia wakati wa utekelezaji wa majukumu yake kwa wananchi pamoja na maelekezo ya Serikali kwa ujumla.
- ii. Mazingatio ya bajeti ya matumizi ya kawaida ni gharama zote za uendeshaji wa ofisi, safari za kikazi, vikao vinavyohusu nje ya sekta na gharama za Mishahara, shughuli zinazotekelezwa zinatakiwa zihusishwe katika viashiria na shabaha za utekelezaji vinavyotokana na ZADep kwenye shughuli kuu (core function).
- iii. Afisa Masuuli anatakiwa kutenga fedha katika upangaji wa bajeti kwa ajili ya mabadiliko Tabianchi na maafa, watu wenye mahitaji maalumu na shughuli muhimu za uendeshaji wa ofisi ikiwemo umeme, maji, simu, ulinzi, usafi pamoja na kulipa madeni ya watumishi, wakandarasi, wazabuni na watoa huduma kwa kuzingatia ukomo uliotolewa.
- iv. Afisa Masuuli anatakiwa kusimamia utaratibu wa uhaulishaji wa vifungu vya matumizi na kufata utaratibu wa matumizi ya fomu na barua za uhaulishaji. Kwa mujibu wa Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka

- 2021 kifungu (20)(1) taratibu za uhaulishaji zitaanza kufanyika baada ya miezi sita (6) ya utekelezaji wa bajeti.
- v. Afisa Masuuli anatakiwa kuwatayarisha maafisa mipango ambao wanashughulikia bajeti kujiandaa na uingizaji wa taarifa katika mfumo mara tu itakapo tolewa ratiba na watatakiwa kuwepo muda wote mpaka litakapomalizika zoezi la uwekaji taarifa katika mfumo.
  - vi. Afisa Masuuli anatakiwa atumie taarifa za matokeo ya Sensa ya watu na Makaazi ya mwaka 2022 katika uandaaji wa mipango na bajeti wakati wa ugawaji wa rasilimali.
  - vii. Kila Taasisi ya Umma inatakiwa kuweka katika bajeti yake maombi ya ununuzi wa gari mpya kwa mujibu wa mahitaji yao na kuyawasilisha maombi hayo Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya ununuzi wa pamoja (Bulk Procurement of Motor Vehicle).
  - viii. Kila Taasisi ya Umma inatakiwa kuvifanyia matengenezo makubwa na madogo (Service) vyombo vya moto kulingana na muongozo kutoka kwa mtengenezaji (Manufacturer).
  - ix. Afisa Masuuli ametakiwa atambue kuwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango itakata gharama za matumizi ya umeme kutoka katika matumizi mengineyo ya Taasisi husika kwa kulipa Madeni ya umeme.
  - x. Taasisi zote zimekatazwa kufunga mikataba yenye kipengele kinachohusisha misamaha ya kodi, kwa sababu jukumu hilo la kutoa misamaha lipo chini ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango (Mikataba inayohusiana na misamaha ya kodi).

### **2.3 Uandaaji wa Bajeti yenye kuzingatia jinsia na usawa (Gender Responsive Budget and Equity)**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (RGoZ) imedhamiria kufanya mageuzi ya bajeti ya Serikali yatakayohakikisha uimarishaji wa usawa wa kijinsia unaokwenda sambamba na dhana ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 Zanzibar (ZADEP), Sera mbalimbali za sekta na utekelezaji wa Lengo Nambari 5 la Maendeleo Endelevu (SDGs).

Katika kufanikisha azma hiyo, bajeti ya Serikali kupitia wizara zote 18 zinatakiwa kutayarishwa kwa kuzingatia dhana ya jinsia itakayohusisha wanawake, wanaume, wasichana, vijana, wazee, walemavu, watoto na makundi mengineyo na mahusiano ya mahitaji yao katika jamii. Dhana ya bajeti ya jinsia inalenga kuimarisha na kuhakikisha kuwa makundi hayo yote yanazingatiwa ipasavyo katika mipango na bajeti za kila wizara ili kuakisi maendeleo ya wazanzibari wote (**no one left behind**) yatakayopatikana kutokana na ukuaji wa uchumi jumuishi.

Wizara hizo zitahusisha baadhi ya majukumu ya msingi katika kufanya uchambuzi wa bajeti inayozingatia jinsia, kuweka makisio ya bajeti pamoja na kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya uidhinishaji.

Kwa Upande wa Utekelezaji wa bajeti ya Serikali, mageuzi hayo yatafanyika kwa Wizara sita za majaribio ambazo ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Afya; Wizara ya Uchumi wa Buluu; Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais, Katiba, Utumishi na Utawala Bora.

Wizara hizo za majaribio zitafanya ufuatiliaji pamoja na uandaaji wa ripoti kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. Aidha, Wizara hizo pia zitafanyiwa ufuatiliaji na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili kupata taarifa za utekelezaji halisi wa bajeti iliyotekelezwa kijinsia.

Maeneo mengine yakuzingatia kwa Taasisi zote ni pamoja na:

- i. Afisa Masuuli anatakiwa kutambua masuala ya kijinsia katika eneo lake la kazi kwa kufanya uchambuzi wa

kijinsia kwa kutumia takwimu ili kutekeleza hatua za kukabiliana na upungufu uliobainika.

- ii. Kuhakikisha vituo vyote vya kutolea huduma, kama vile nyumba za wazee, skuli, hospitali na ofisi vinafikika na watu wote ikiwemo wenye mahitaji maalumu.

Muundo na maelekezo ya uandaaji wa Bajeti ya jinsia umeambatishwa **Kiambatisho Namba:5**

## **2.4 Upangaji wa Bajeti za Mishahara**

Katika uandaaji wa Bajeti ya mishahara kwa watumishi tunapaswa kuzingatia kufanya marekebisho ya bajeti za posho la likizo kwa Wakurugenzi Wakuu, Makamishna, Maafisa Wadhamini, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi na Manaibu Wakurugenzi wa Taasisi zinazopokea Ruzuku na zile zinazojitegemea na Watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa toleo lenye kumbukumbu namba CAB.78/388/01/11 la tarehe 04 Disemba 2023 kutoka Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

- i. Afisa Masuuli anatakiwa kusimamia miiko ya utumishi wa Umma kanuni ya 32G inawataka watumishi wote wa Umma ambao wanachukua mkopo bakaa ya makato yake yasipungue theluthi mbili (2/3) ya mishahara wake.
- ii. Afisa Masuuli anatakiwa kupanga bajeti inayozingatia malipo ya posho la madereva na makatibu muhtasi wa viongozi wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa toleo lenye kumbukumbu namba CAB.78/388/01 la tarehe 04 Disemba 2023 kutoka Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.
- iii. Afisa Masuuli anatakiwa kuwasilisha maombi ya bajeti za mishahara ya ajira mpya Afisi ya Rais Fedha na Mipango mara tu atakapopata muongozo huu, maombi

haya ni kwa ajira ambazo zimeshapatiwa kibali kutoka Tume za Utumishi.

- iv. Afisa Masuuli anatakiwa kuhakikisha ya kwamba mshahara wa watumishi wanaopata uhamisho wa taasisi unabakia katika taasisi za awali hadi utakapoingia mwaka mpya wa fedha, agizo hili halitowahusu watumishi watakaopata uteuzi.
- v. Afisa Masuuli anatakiwa kuzingatia upangaji wa mishahara na maposho ya watumishi kwa mgawanyo wa programu kuu na programu ndogo.
- vi. Kwa taasisi ambazo zina wafanyakazi waliopangiwa katika ofisi za Pemba na hawana vocha za mishahara kwa upande wa Pemba wanatakiwa kuwasilisha orodha za watumishi hao Ofisi ya Rais Fedha na Mipango katika kitengo cha mishahara ili waweze kutengenezewa vocha za Pemba.
- vii. Afisa Masuuli anatakiwa kulipa stahiki za kisheria kwa watumishi ikiwemo posho za likizo na posho za wito wa madaktari ili kuepuka uzalishaji wa madeni.
- viii. Afisa Masuuli anatakiwa kuhakikisha upangaji wa gharama za Mishahara unaozingatia mahitaji halisi waliyoomba kwenye Bajeti yakiwemo mazingatio ya watumishi katika eneo la masomo, ongezeko la mishahara, wastaafu na ajira mpya ili kuepusha matumizi makubwa ya Fungu la Marekebisho ya Mshahara (salary adjustment);
- ix. Afisa Masuuli anatakiwa kuondoa na kutoruhusu mikato yote isiyo ya kisheria katika mishahara, mfumo mpya wa **HRMS na PAYROLL** ambao unatarajiwa kutumika katika mwaka wa Fedha 2024/2025, hautaruhusu makato mengine yasiyokuwa ya kisheria.

## **2.5 Maelekezo ya Utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2024/25**

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25 Wizara, Idara na Taasisi za Serikali pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo katika utayarishaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo unaosimamiwa na Tume ya Mipango:-

- i. Miradi itakayowasilishwa kwa utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 izingatie Muongozo wa uandaaji wa Miradi ya Serikali na maboresho yake kama ilivyoelekezwa na Tume ya Mipango Zanzibar;
- ii. Miradi itakayowasilishwa izingatie maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii kwa kupunguza umaskini na kuimarisha utoaji wa huduma za jamii;
- iii. Miradi itakayowasilishwa iwasilishwe sambamba na Mpango Mkakati wa Wizara husika unaoendana na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026);
- iv. Sekta zihakikishe kuwa wanaweka kipaumbele kutekeleza miradi inayoendelea kabla kuanza utekelezaji wa miradi mipya;
- v. Wizara na Taasisi kuandaa miradi kwa kuzingatia taarifa za upembuzi yakinifu ili kuepusha mabadiliko ya mara kwa mara yanayopelekea kuongezeka gharama za utekelezaji wa miradi hiyo;
- vi. Ugawaji wa rasilimali utazingatia maeneo ya vipaumbele kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026);
- vii. Ugawaji wa rasilimali utazingatia zaidi kipaumbele kwenye miradi ya kimkakati, hivyo mipango na shughuli zote za sekta ziendane na Mpango Mkakati wa Wizara/Taasisi pamoja na maelekezo ya Serikali Kuu;
- viii. Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinazopokea fedha za programu na miradi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, kuwasilisha Mpango wa fedha hizo Tume ya

- Mipango mara tu baada ya kuthibitishwa na Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango Kupitia Idara ya Fedha za Nje;
- ix. Maagizo yanayotolewa kutoka Serikalini yanayohusu kuanzisha kwa mradi, taasisi husika inawajibika kufuata taratibu zilizowekwa ikiwemo kuandaa andiko la mradi pamoja na kutambua vyanzo vya fedha vitakavyotumika kwenye ufadhili wa mradi husika, kabla ya kuwasilishwa Tume ya Mipango kwa maombi ya kupatiwa fedha;
  - x. Utoaji wa fedha utazingatia mahitaji ya matayarisho ya awali ya mradi ikiwemo kazi za uandaaji wa mikataba, michoro, ‘BoQ’ na utangazaji wa zabuni, sekta husika zitatekeleza kazi hizo kupitia fedha za matumizi ya kawaida na hakutokuwa na utoaji wa fedha za mradi wowote kabla ya kukamilika matayarisho hayo;
  - xi. Kupanga mipango ya maendeleo kwa weledi na uhakika ili kuepusha uhaulishaji wakati wa utekelezaji wake; na
  - xii. Kuwasilisha bajeti zilizo na uhalisia kwa lengo la kupelekea mgawanyo mzuri wa rasilimali fedha.
  - xiii. Bajeti kuzingatia Mkakati Endelevu wa Kifedha kwa Miradi ya Maendeleo **(Kiambatisho Namb 6)**

## **2.6 Upangaji wa Bajeti kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo**

Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinazopokea fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, zinatakiwa kuwasilisha Mipango na Bajeti ya fedha zinazotumika kwa Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo; fedha hizo zinatakiwa kuwasilishwa kwa makisio na mchanganuo wa upatikanaji wa fedha hizo kwa Kipindi cha Miaka Mitatu (MTEF) 2024/2025-2026/2027.

Mchanganuo huo ujumuishe fedha za namna nne zifuatazo;

- a. Fedha zinazoingia katika akaunti za Wizara au Serikali (Special Account)

- b. Fedha zinazolipwa kwa mkandarasi au mshauri elekezi atakae ajiriwa na washirika wa maendeleo moja kwa moja (Direct Payment)
  - c. Fedha zinazolenga kusaidia bajeti ya Serikali (Budget Support)
  - d. Thamani ya fedha katika matumizi ya Serikali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa mchango usiokuwa wa fedha (Contribution in kind) na fedha za Matumizi ya Kawaida (recurrent expenditure) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinatakiwa kuwasilishwa wakati wa maandalizi ya bajeti ili zijumuishwe katika bajeti za taasisi husika.
- i. Sekta inayotegemea kupanga miradi ambayo upatikanaji wa fedha unategemea zaidi mkopo wa biashara kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Sovereign Guarantee), inapaswa kutambua na kufahamu kuwa kabla ya kuwasilisha maombi yake Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Idara ya Fedha za Nje kuhakikisha kuwa;
- a. Imeufanyia upembuzi yakinifu mradi wake;
  - b. Imefanya mpango wa kimazingira mradi wake (ESIA);
  - c. Kwa miradi inayohusu ujenzi ambao kwa namna moja au nyengine itahusisha uondoaji wa watu, taasisi husika inapaswa kuandaa mpango wa kulipa fidia (RAP Assessment) na kuhakikisha Serikali imetenga fungu maalumu kwa ajili ya ulipaji wa fidia kuepusha ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi.
  - d. Miradi inayoendelea kwa kila sekta inatakiwa kuwa na andiko la mradi husika. Miradi ya muda mrefu ambayo haijamalizika inatakiwa kufanyiwa mapitio ili kuainisha fedha zinazohitajika kwa kumalizia shughuli za asili za mradi huo. Inasisitizwa kuwa shughuli mpya tofauti na zilivyoainishwa katika andiko la asili hazitokubalika.



- ii. Afisa Masuuli anapaswa kutambua na kufahamu kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma No.16 ya mwaka 2016 Ibara No. 58(1) na Ibara ndogo (3) ya sheria hii ambayo inampa mamlaka kisheria Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuwa, masuala yote yanahusu utafutaji wa rasilimali fedha Nje ya Nchi yapo chini yake, na kwamba endapo taasisi kupitia Afisa Masuuli amepokea fedha au msaada wa aina yoyote atapaswa kuwasilisha taarifa hizo kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kabla ya kuanza matumizi ya Fedha hizo au msaada huo wa kiufundi.
- iii. Afisa Masuuli anaweza kufanya mazungumzo ya awali kwa kushirikiana na Idara ya Fedha za Nje kwa ajili ya kuomba msaada au mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo, hairuhusiwi Taasisi yoyote Serikalini kuingia Mikataba ya Makubaliano na Washirika wa Maendeleo ya kupokea misaada ya fedha au misaada ya kiufundi na mikopo pasipo idhini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha.
- iv. Afisa Masuuli anatakiwa kuwasilisha makadirio ya bajeti na takwimu za ahadi za fedha za nje katika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango katika Idara ya Fedha za Nje ili kukamilisha maandalizi ya ukomo wa bajeti za mafungu.
- v. Taasisi za Serikali zinazotarajia kupokea mikopo, misaada na zinazohitaji Dhamana ya Serikali zinapaswa kupata idhini kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha, kwa mujibu wa kifungu cha 58(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 baada ya kupitiwa na Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa. Uwepo wa Deni la Taifa umetajwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Sura ya 7 Ibara ya 110 (1) (2).
- vi. Upangaji wa miradi mipya Sekta zinatakiwa kuzingatia Muongozo wa Uandaaji Miradi na Majadiliano ya Mikopo

na Upokeaji wa Misaada uliotolewa na Idara ya Fedha za Nje-ORFM pamoja na kuzingatia Sheria ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) ya mwaka 1998, Jadweli namba 3 zinazoelekeza utoaji wa Msamaha wa VAT kwa Taasisi zinazotekeleza miradi iliyopo chini ya ufadhili wa fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo.

- vii. Kwa mradi unaotekelezwa kwa namna moja au nyengine utahusisha ubia na sekta binafsi, sekta inapaswa kutambua kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi husika imefanya tathmini ya kutosha juu ya mgawanyo wa mapato yatokanayo na mradi kati ya Serikali na Mbia, na kuhakikisha kuwa mradi huo umefata taratibu zote zilizopo za sheria ya PPP.
- viii. Upangaji wa Programu uzingatie shughuli kuu za Taasisi husika kwa kuleta matokeo ya muda mfupi na mrefu (outputs and outcomes) na malengo ya Taasisi.
- ix. Miradi inayoendelea kutekelezwa kupewa kipaumbele katika kutengewa fedha kwa ajili ya kuikamilisha kabla ya kuanza miradi mipya. Aidha, Wizara ambazo zinaratibu miradi na programu zinazoshirikisha utekelezaji wa Mafungu mengine kuhakikisha bajeti za miradi hiyo zinatengwa katika Mafungu husika.

**TANBIHI:** Kwa hali yeyote ile hairuhusiwi kwa sekta kupokea au kuidhinisha fedha za washirika wa maendeleo pasina idhini ya Waziri mwenye dhamana ya Fedha Zanzibar.

## **2.7 Maelekezo kwa Taasisi zinazojitegemea na Mashirika ya Umma**

- i. Maafisa Watendaji Wakuu wa Taasisi za Uwekezaji za Umma wanatakiwa kutofanya matumizi ambayo

hayajaidhinishwa na Bodi za Wakurugenzi, na kwa mujibu wa kifugu 26 (1)(b) cha sheria ya Msajili wa Hazina Nam. 6 ya mwaka 2021 ni kinyume cha sheria na ikibainika na kuthibitika matumizi yamefanyika watawajibishwa kibinafsi kwa matumizi hayo.

- ii. Mashirika yote ya Uwekezaji wa Umma yanatarajiwa kutoa mapato yanayoridhisha, kutangaza na kulipa gawio kwa Serikali kama ilivyoelezwa katika kifungu 41 (1) (b) cha sheria ya Msajili wa Hazina Nam. 6 ya mwaka 2021. Katika suala hili, Taasisi za Uwekezaji za Umma zinahitajika kufata Sera ya Gawio na kuwasilisha kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuidhinishwa.
- iii. Mashirika yote ya Uwekezaji wa Umma yanatakiwa kufuata sheria na taratibu za kukopa kwa mujibu wa Kifungu cha 58 (6) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, 2016; na iwapo inaruhusiwa na sheria nyingine bila ya kukinzana na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, 2016.
- iv. Mashirika yote ya Uwekezaji wa Umma yanatakiwa kuwasilisha taarifa zote muhimu zinazohitajika katika uwasilishaji wa makadirio ya bajeti ya mwaka 2024/2025 katika vielelezo vilivyoambatanishwa katika muongozo uliotolewa na Msajili wa Hazina 25, Septemba 2023.
- v. Mashirika yote ya Uwekezaji wa Umma yanatakiwa kuandaa ripoti ya utekelezaji wa bajeti ya kila robo mwaka katika muundo kama ilivyoelekezwa katika kifungu 43 cha sheria ya Msajili wa Hazina. Ripoti itaonyesha hali ya utekelezaji wa bajeti ya mapato, bajeti ya matumizi na utekelezaji wa mradi.

vi. Mashirika yote ya Uwekezaji wa Umma yanatakiwa kuwasilisha mapato yote yanayopatikana kwa taasisi husika, ikijumuisha Ruzuku/Ufadhili wa Serikali na Mkopo katika Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa muda na tarehe zilizoainishwa katika Muongozo uliotolewa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar.

### **3 Maelekezo Maalumu Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2016, kifungu namba 86(4), Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inahusika na kutoa muongozo wa bajeti kwa ajili ya utayarishaji wa bajeti kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inahusika na kutoa rasilimali fedha kwa taasisi hizo kulingana na uwezo wa kifedha wa Serikali kwa kuzingatia bajeti iliyopitishwa na Mabaraza ya Madiwani.

#### **3.1 Maelekezo ya Bajeti kwa Vianzio vya Mapato vya Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM)**

Maandalizi ya Mipango na Bajeti hutegemea kwa sehemu kubwa mapato kupitia vyanzo vya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa husika. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kukusanya mapato kwa njia ya kielektroniki ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Mapato hayo yanatakiwa kupangiwa matumizi mbalimbali kwa mujibu wa utekelezaji wa mpango mkakati wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na maelekezo yaliyotolewa na Serikali kuu katika muongozo huu.

#### **3.2 Maelekezo ya Matumizi ya Fedha za Ruzuku kwenda Serikali za Mitaa**

Matumizi ya fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu yanalenga kuimarisha huduma za jamii na kiutawala kwa ulipaji wa

mishahara inayohusisha wafanyakazi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinapaswa kutenga asilimia isiyopungua 30 ya makusanyo ya mapato zitakazotumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### **3.3 Fedha za Washirika wa Maendeleo**

Fedha za Washirika wa Maendeleo ni chanzo chengine cha mapato ya MSM ambapo, fedha hizo zinatakiwa kutumika katika Matumizi ya kazi za Maendeleo na kutotumika katika shughuli za matumizi ya kazi za kawaida (Recurrent). Miradi yote inayotokana na Fedha za Washirika wa Maendeleo inatakiwa kuripotiwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Idara ya Fedha za Nje na Tume ya Mipango katika muda wa maandalizi ya Bajeti. Endapo zitatolewa fedha za washirika wa maendeleo baada ya kipindi cha kuingiza taarifa za bajeti kumalizika, taarifa za fedha hizo ziwasilishwe OR-Fedha na Mipango kwa kupata maelekezo ya matumizi ya fedha hizo.

**TANBIHI:** Inasisitizwa kuwa fedha zote zinazopokelewa moja kwa moja au kwa kupitia utekelezaji wa mradi kwa aliyeajiriwa na Washirika wa Maendeleo kama vile UNICEF, UNFPA, UNWOMEN na wengineo, kuhakikisha kuwa fedha hizo zinariportiwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango katika Idara ya Fedha za Nje kwa kuzingatia matumizi na taratibu zilizopo.

### **3.4 Fedha za Mikopo**

Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinaweza kukopa fedha zinazopatikana kwa njia ya mkopo kutoka kwa taasisi mbalimbali za kifedha kwa kupitisha maombi kwa Katibu Mkuu mwenye dhamana na baadae maombi hayo kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kama taratibu zinavyoeleza.

### **3.5 Fedha za Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo**

Fedha za Mfuko wa Jimbo ni miongoni mwa vyanzo vya ndani vya mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Fedha hizo zinajumuisha kutoka mfuko wa Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mfuko kutoka Ofisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Kutokana na vikao na mijadala mbalimbali iliyofanyika baina ya Serikali Kuu na MSM imekubalika kuwa fedha hizi hazitafanyiwa makadirio wakati wa upangaji. Hata hivyo, fedha hizo zinatakiwa kuandikiwa ripoti wakati wa upokeaji pamoja na matumizi yake na kuwasilishwa katika ngazi zote kama utaratibu wa uwasilishaji wa ripoti za mapato na matumizi unavyoelekeza.

Fedha za maendeleo za mfuko wa jimbo zinatakiwa zitumike kwa kuzingatia vipaumbele vya wananchi wanavyoibua kupitia Mabaraza ya Wadi na Kamati za Mashauriano za Shehia.

### **3.6 Maelekezo Mengine kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Afisa Masuuli ambao ni wasimamizi wa shughuli zilizopangwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

- i. Kuhakikisha kuwa mifumo ya kielektroniki inatumika katika makusanyo ya mapato na matumizi wakati wa uandaaji wa bajeti, na Utekelezaji wa Bajeti za MSM;
- ii. Fedha zilizopangwa kwa utekelezaji wa Kazi za Maendeleo haziruhusiwi kutumika katika matumizi ya Kazi za Kawaida;
- iii. Katika mipango ya mwaka kuwepo na fedha asilimia 10 ambazo zitasaidia kuchangia katika mfuko wa uwezeshaji

- wananchi kiuchumi kwa lengo la kusaidia makundi maalumu wakiwemo wanawake na watu wenye mahitaji maalumu kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu na kuinua vipato ili kupunguza umasikini;
- iv. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kutekeleza miradi mbali mbali iliyoibuliwa na wananchi katika shehia zao, ikiwemo miradi ya uendelezaji wa miji, ujenzi wa madarasa, ujenzi wa vituo vya afya, vyoo vya jamii, masoko, vituo vya abiria, upatikanaji wa maji safi na salama, machinjio, usafishaji wa mazingira kwa ajili ya kuimarisha ustawi wa wananchi katika jamii;
  - v. Kutenga fedha kwa ajili ya kusaidia maafa yanayotokea katika maeneo ya Serikali za Mitaa.
  - vi. Kuwatambua na kuwasajili wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo kwa kuwapatia vitambulisho na kuwawezesha kufanya shughuli za biashara katika mazingira rafiki katika eneo la Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuongeza mapato.
  - vii. Fedha za Bajeti kwa mwaka 2024/2025 zitumike kwa utaratibu ufuatao:
    - a. Asilimia 30 zielekezwe katika matumizi ya Miradi ya Maendeleo;
    - b. Asilimia 30 zielekezwe katika kazi za Usafi wa Miji;
    - c. Asilimia 30 zielekezwe katika kazi za kawaida na
    - d. Asilimia 10 zielekezwe katika uwezesaji kiuchumi kwa makundi maalumu (Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu).

#### **4 MAELEKEZO YA ZIADA KWA TAASISI AMBAZO ZINAPOKEA RUZUKU**

Serikali inaendelea kuweka uwiyo wa bajeti katika matumizi ya kawaida kwa kupunguza bajeti ya matumizi

mengineyo kwa taasisi zinazopokea ruzuku na kuongeza bajeti ya mishahara lengo ni kuboresha maslahi ya watumishi.

Taasisi za ruzuku zinatakiwa kuandaa bajeti kwa kuhusisha Mpango Mkakati (Strategic Plan), Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) na kufuata Mfumo wa Bajeti inayozingatia Programu (PBB) pamoja na kuhusisha shughuli zote za taasisi na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika maeneo yao sambamba na kuzingatia ahadi za Mheshimiwa Rais katika maeneo wanayoyasimamia. “Taasisi zote zinazopokea Ruzuku zinatakiwa kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha miezi nane Julai hadi Febuari mwaka 2023/2024 kwa mchanganuo wa vianzio vya Mapato na Matumizi kabla ya uwasilishaji wa Bajeti.” Aidha, Taasisi hizi zinatakiwa kusimamia vizuri makusanyo ili kukidhi nakisi ya bajeti zao kwa lengo la kujitegemea.

Taasisi za ruzuku zinatakiwa kuzingatia ipasavyo maelekezo yatakayotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ili kwenda sambamba na azma ya Serikali ya kuwa na bajeti ya mfumo mmoja kwa taasisi zote za Serikali.

Kwa matayarisho ya Bajeti ya mwaka 2024/2025, taasisi zote zinazopokea ruzuku zitatakiwa kuingiza taarifa za bajeti katika mifumo iliyopo (BAMAS) kwa kuingiza uchambuzi wa vifungu vya Bajeti kama utaratibu uliotumika mwaka jana.

## **5 UANDAAJI NA UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI**

Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2016 Kifungu cha(53)(1-3) Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa na kuwasilisha, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, taarifa za utekelezaji wa bajeti kila robo mwaka ndani ya siku



thalathini 30 baada ya kukamilika kwa robo ya mwaka husika.

Aidha taarifa za utekelezaji wa bajeti za Mwaka ziwasilishwe ndani ya mwezi wa Oktoba baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha husika. Uwasilishaji huu wa taarifa za utekelezaji wa bajeti uwe kwa nakala ngumu na nakala laini kupitia email [staff.bajeti@mofzanzibar.go.tz](mailto:staff.bajeti@mofzanzibar.go.tz) Fomu ya uwasilishaji wa taarifa za Utekelezaji wa bajeti **Kiambatisho Namba:5**

**TANBIHI:**

Wizara, Idara na Taasisi ambayo ina mahitaji ya bajeti ya ziada kwa mujibu wa ukomo uliotolewa, kwa ajili ya utekelezaji wa agizo la Serikali au Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2024-2025 ambapo kiuhalisia mahitaji ya Bajeti ya kutekeleza eneo hilo gharama zake ni kubwa na haijazingatiwa katika makadirio ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo, atahitajika kuleta mapema gharama za utekelezaji wa shughuli hiyo pamoja na matokeo (out put and out come result) kabla ya kikao cha Majadiliano ya Bajeti (Bugdet Dialogue).

Wakuu wa mafungu yaliyomo katika Bajeti ya Serikali, Wakuu wa Taasisi zinazopokea Ruzuku kutoka Serikalini, Mamlaka za Serikali za Mitaa, naomba tupokee muongozo huu na kuendelea na matayarisho ya Bajeti kwa mwaka 2024/2025.

Ahsante

DKT. JUMA MALIK AKIL  
**MLIPAJI MKUU WA SERIKALI  
ZANZIBAR.**

**Nakala:**

**Mhandisi. Zena Ahmed Said**

Katibu wa Baraza la Mapinduzi na  
Katibu Mkuu Kiongozi,  
**Zanzibar.**

**6 VIAMBATISHO**

- Kiambatisho namba 1: Kalenda ya Bajeti  
Kiambatisho namba 2: Kasma za Bajeti  
Kiambatisho namba 3: Muundo wa Mpango Kazi.  
Kiambatisho namba 4: Muundo wa utayarishaji wa Bajeti inayozingatia jinsia na usawa  
Kiambatisho namba 5: Fomu ya uwasilishaji wa Taarifa za utekelezaji wa bajeti  
Kiambatisho namba 6: Bajeti kuzingatia Mkakati Endelevu wa Kifedha kwa Miradi ya Maendeleo

<b>Kimbatisho Namba:1 KALENDA YA MPANGO NA BAJETI KWA UTEKELEZAJI WA MWAKA 2024/2025</b>	
<b>MUDA WA UTEKELEZAJI</b>	<b>SHUGHULI HUSIKA</b>
<b>Julai</b>	Kuhamisha bajeti kupelekwa katika mfumo wa Matumizi baada ya Kuidhinishwa BLW
	<b>Kuwasilishwa Maombi ya Idhini ya Matumizi kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)</b>
<b>Agosti</b>	Kutoka kwa Ripoti ya mwaka ya Mishahara
	Ukusanyaji wa Taarifa za Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka uliopita
<b>Septemba/Oktoba</b>	Uwasilishaji wa Maombi ya Miradi ya Maendeleo
	Uandishi wa Ripoti za Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka
	<b>Kuwasilishwa Maombi ya Idhini ya Matumizi kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)</b>
	<b>Mkutano wa Kujadili taarifa za Majibu ya Ripoti za Kamati zilizowasilishwa katika Mkutano uliopita (BLW)</b>
	Uwasilishaji wa Ripoti za Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka Uliopita kwa Kamati Tendaji
	Kukutana na Taasisi kwa Mijadala ya Fedha za Washirika wa Maendeleo
<b>Novemba /Disemba</b>	Uandishi na Uwasilishaji wa Ripoti ya utekelezaji wa bajeti ya robo mwaka (Mwaka wa fedha husika)
	Kufanya Mapitio ya Bajeti ya Makisio ya miezi sita na kutizama mapungufu yaliyojitokeza
	<b>Mkutano wa Kujadili Miswada ya Sheria ya Serikali (BLW)</b>
	Uwasilishaji wa Taarifa za Maombi ya Miradi Tume ya Mipango
	Majadiliano ya Miradi ya Maendeleo kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali
	Kukusanya taarifa kwa ajili ya Maandalizi ya Mpango na Mwelekeo wa Bajeti
<b>Januari</b>	Kuandaa Muongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa maendeleo na Bajeti kwa Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa
	<b>Kuwasilishwa Maombi ya Idhini ya Matumizi kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)</b>
	Jukwaa la Uchumi na Bajeti kwa Serikali kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa
	Kuandaa mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali
	Kikao cha Majadiliano ya Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Makatibu wakuu (IMTC)
	Majadiliano ya Mipango ya Maendeleo ya Serikali
Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali Kuwasilishwa Baraza la Mapinduzi Kujadiliwa	

	Uwasilishaji wa Mapendekezo ya Miradi kwa Mara ya Pili
	Kuandaa mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali na kuwasilishwa Baraza La Wawakilishi kujadiliwa
	Uwasilishaji wa Mapendekezo ya Miradi kwa Mheshimiwa Rais kwa Kupata Idhini
	Mafunzo yanayohusu Bajeti kwa Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa
	Kuandaa Muongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa maendeleo na Bajeti kwa Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa
Mwezi wa Februari	Mijadala na Mashauriano ya Mipango na Bajeti kuhusu ukomo wa mgao wa bajeti (Wizara, Idara na Taasisi za Serikali)
Mwezi Februari	Mkutano wa Kujadili Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, 2023/24
	Kujadili Muelekeo wa Mpango wa Taifa, 2024/25 (BLW)
	Uwasilishaji wa Bajeti za Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MTEF) ORFM
Mwezi wa Machi	Kuwasilishwa Maombi ya Idhini ya Matumizi kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)
	Uingizaji wa Taarifa za Bajeti katika Mfumo wa Bajeti (ISIDORE)
Mwezi wa Aprili	Kuwasilishwa kwa Mswada wa Mipango na Bajeti katika Kamati za Kudumu za Bajeti (BLW)
	Mijadala ya Mipango na Bajeti kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali (BLW)
	Kutayarishwa kwa Mswada wa Sheria ya Fedha
Mwezi wa Mei	Kutayarishwa kwa Mswada wa Sheria ya Matumizi
Mwezi Mei na Mwezi Juni	Mkutano wa Kujadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2024/25 BLW
	Kuwasilisha Mwelekeo wa mpango wa maendeleo for FY 2024-2025
	Kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya seikali For FY 2024-2025
	Kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Mapato kwa Kamati ya Bajeti ya BLW
Mwezi wa Juni	Kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Mapato na Mswada wa sheria ya Matumi katika Baraza la Wawakilishi

2201014	Small Engineering Tools and Equipment	Vifaa vidogovidogo vya Uhandisi
2201015	Trainees Equipments	Vifaa vya Wanafunzi
2201016	Purchase of mattresses	Ununuzi wa magodoro
2202001	Food and Refreshment	Chakula na Vinywaji
2202002	Refreshment	Viburudishaji
2202003	Gifts/ prizes	Ununuzi wa Zawadi
2202004	Transport / Lunch	Usafiri / chakula
2202008	Radio Call	Radio koli
2202009	Porriage Expenses Pre Primary	Gharama za Uji Maandalizi
2202010	Porriage Expenses Primary	Gharama za Uji Msingi
2202011	Trainees Cuttering Services	Chakula cha Wanafunzi na Mahabusu
2202012	Purchase of Identification Card	Ununuzi wa Vitambulisho
